

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MIRADI YA UBIGI SEKTA YA UMMA NA BINAFAZI CHACHU YA MAENDELEO  
YA UCHUMI WA VIWANDA**

Sekta Binafasi inamchango mkubwa katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi yatakayoiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati unaotegemea viwanda iwapo itashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya Sekta ya umma na binafasi (PPP).

Hayo yamebainishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Bw. Doto James, katika Semina ya Ubigi kati ya sekta ya Umma na sekta Binafasi (PPP) iliyowakutanisha makatibu wakuu, wakuu wa taasisi, na watendaji wa Serikali Jijini Dar es Salaam.

Bw. James alisema kuwa Serikali imeweka mfumo wa kisera, kisheria na kitaasisi pamoja na kanuni zake ili kuweka mazingira wezeshi ya kuongeza ushiriki wa Sekta Binafasi katika kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo.

‘Lengo la Semina hii ni kupata uelewa kuhusu masuala muhimu ya kuzingatia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa ubigik kwa dhamira ya kuchangia jitihada za kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano kuanzia 2016 hadi 2020 ili kuweza kufikia uchumi wa viwanda” alieleza Bw. James.

Aidha aliwataka wadau katika semina hiyo kuhakikisha wanawajibika kikamilifu kuchambua na kufuata hatua zote muhimu za utekelezaji wa miradi ya Ubigi kati ya Serikali na Sekta Binafasi-PPP, kwa kuwa hatua hiyo itaiwezesha Serikali kupata miradi ya maendeleo yenye sifa na ubora unaotakiwa nchini.

Katibu Mkuu huyo alitaja baadhi ya miradi ambayo inatekelezwa kwa utaratibu wa PPP kuwa ni pamoja na mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri Jijini Dar es Salaam Awamu ya kwanza (UDART) ambao uko katika hatua ya utekelezaji.

Aliongeza kuwa, miradi mingine ambayo iko katika hatua za mwisho za upembuzi yakinifu ni pamoja na mradi wa kuzalisha madawa muhimu na vifaa tiba na mradi wa ujenzi wa Vyuho Kumi (10) vya Ufundi Stadi unaotekelezwa na VETA.

Miradi ambayo ipo katika hatua ya kuandaa taarifa za maandiko ya awali alisema kuwa ni pamoja na mradi wa kusambaza gesi nchini ambao utatekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), mradi wa kujenga mabweni ya wanafunzi utakaotekelezwa na Chuo cha Elimu ya Biashara- CBE na mradi wa kujenga taasisi ya Taifa ya Saratani utakaotekelezwa na *Ocean Road Cancer Institute*.

‘Maandalizi ya miradi hiyo ambayo ipo katika hatua ya kuandaa taarifa za maandiko ya awali itakapo kamilika itatekelezwa na wabia kutoka Sekta binafsi watakaokuwa wamepatikana kwa wakati huo’, alifafanua Bw. James

Nae Kaimu Mkurugezi wa mkondo wa chini wa Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), Emmanuel Gilbert, alisema kuwa uwekezaji kwenye usambazaji wa mafuta na gesi hapa nchini kwa utaratibu wa PPP, utasaidia wananchi kuweza kutumia gesi ya hapa nchini kwa haraka.

Alisema katika mradi huo wa kusambaza gesi utashirikisha waombaji watakao kidhi vigezo kwa ajili ya usambazaji wa gesi hiyo, aidha alibainisha vituo vya usambazaji kwa jiji la Dar es Salaam kuwa vitakuwepo katika Manispaa ya Ilala, Temeke na Kinondoni.

**Imetolewa na;**

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Wizara ya Fedha na Mipango**